





Mkahawa huzaa matunda
yaliyo na mbegu ndani.

Mbegu hizo ni kahawa.






Kuna hekaya nyingi kuhusu
jinsi kahawa
ilivyogunduliwa. Mojawapo
inamhusu Kaldi, raia wa
Ethiopia.



Kaldi alikuwa mchungaji
nchini Ethiopia.



Inasemekana kuwa siku
moja mbuzi wake waliyala
matunda ya rangi nyekundu
kutoka mti wa kahawa.


Baadaye, Kaldi alishuhudia
mbuzi hao wakirukaruka
kwa uchangamfu usiokuwa
wa kawaida.




Kaldi alikuwa na hamu
kubwa ya kutaka kujua ikiwa
matunda yale yaliwapa
mbuzi wake nguvu fulani.



Alionja ladha yake chungu
alipoyatavuna.
Baadaye, Kaldi alikuwa
macho. Yeye pia alihisi
nguvu fulani mpya.



Alichuma baadhi ya majani
na yale matunda.




Aliyapeleka nyumbani na kumpatia mkewe.




Mkewe alipoyatavuna yale
matunda, naye pia
aliathirika kama Kaldi.
Alikuwa macho na kuhisi
nguvu ya kipekee.




Kaldi na mkewe waliamini
kuwa matunda yale
yalikuwa zawadi kutoka kwa
Mungu.




Siku chache baadaye, Kaldi
aliwapelekea watawa
matunda yale na majani
yake.



Aliwahadithia jinsi mbuzi
wake walivyoathirika
walipoyala matunda yale.





Alipoondoka, watawa wawili
walimfuata kisirisiri
wakitaka kujua ikiwa ilikuwa
ukweli.



Walihakikisha walipowaona
mbuzi wakichangamka na
kucheza baada ya kuyala
yale matunda.




Watawa walirudi nyumbani
na kuyachemsha yale
matunda ya kahawa.



Walipoyanya maji yaliyochemka, ladha yake ilikuwa chungu sana!
Walidhani kuwa kilikuwa kinywaji cha shetani.



Waliyatupa matunda
yaliyobaki kwenye moto.
Yalipochomeka, walinusu
harufu yake nzuri.



Walipata wazo la kuzikaanga zile mbegu kwanza kabla ya kuzichemsha.



Kinywaji kilichotoka kwenye
mbegu zilizokaangwa
kilikuwa na ladha nzuri zaidi.
Baada ya watawa kunywa
kinywaji kile, walikuwa
macho na wenyewe nguvu.

Tangu wakati huo, watu
hunywa kahawa ili kuwa
macho na pia kuburudika.





Kwa hivyo, unywaji wa
kahawa ulianzia nchini
Ethiopia na kuenea
ulimwengu mzima!

